

NASEMA ASANTE MUNGU

(Kushukuru/Tafakari)

Deogratias Rwechungura

♩. = 90

1. Mungu wangu we wendi we ki ngaya ngu ka ti ka ha ta ri zo te za du ni a
Wa ni e pu shama ba ya ki la si ku ha ta bi la ya ku o mbawa ni ki nga

Nase ma A sa nte EeMu ngu A sa nte A sa nte na ku shuku ru
A sa nte A sa nte sa - na A sa nte kwaku ni pe nda
A sa nteMu ngu A sa nte sa na Mu ngu

CHE ZA KINANDA KABLA YA UBETI UNAOFUATA

2. Nilalapo najikuta usingizi, wala bila ya kujua muda gani;
Najikuta asubuhi kumekucha, bila ya kujua yaliyotokea - Nasema....
3. Wanielekeza kwenya kazi zangu, wanijalia riziki kwa upendo;
Hewa nzuri naivuta bila kodi, ungedai ningelipa nini Mungu - Nasema....
4. Siku zinapita wiki na miezi, yote naiona ni halali yangu;
Na miaka nayo pia inapita, mara chache nakumbuka kushukuru - Nasema
5. Nikiwaza ndugu pia marafiki, baadhi hawapo nami duniani;
Mimi umenijalia afya njema, hayo yote ni mapenzi yako kwangu - Nasema
6. Siyo kwamba mimi ni mkamilifu, ni huruma yako Baba yanilinda,
Yote ninayokutendea kinyume, hujawahi Baba nilipa kisasi - Nasema
7. Nikulipe nini Mimi Mungu wangu, wema wako kwangu kweli wa ajabu,
Unge sema nikulipe Mungu wangu, aibu ingenipata ningeshindwa - Nasema..